


**Afisi ya Msimamizi wa Maagizo ya Umma (OSPI)  
Uchunguzi wa Lugha ya Nyumbani**

<b>Jina la Mwanafunzi:</b>		<b>Tarehe:</b>
<b>Tarehe ya Kuzaliwa:</b>	<b>Jinsia:</b>	<b>Gredi:</b>
<b>Fomu Imekamilishwa na:</b>		
Jina la Mzazi/Mlezi _____ Uhusiano na Mwanafunzi _____		
Saini ya Mzazi/Mlezi _____		
Kama inapatikana, ni lugha gani ungependelea kupokea mawasiliano kutoka kwa shule? _____		
<b>Je, mtoto wako alipokea usaidizi wa kukuza lugha ya Kiingereza kupitia Mpango wa Mpito wa Maagizo ya Lugha mbili katika shule ya mwisho ambayo mtoto wako alihudhuria? Ndiyo__ Hapana__ Sijui__</b>		

1. Je, ni nchi gani mtoto wako alizaliwa?	_____
2. <b>Ni lugha gani ambayo mtoto wako alijifunza kwanza kuongea?*</b>	_____
3. <b>Ni lugha gani ambayo <u>MTOTO WAKO</u> anatumia sana nyumbani?*</b>	_____
4. Ni lugha gani ambazo <u>mzazi/mlezi</u> wanatumia sana wakati unaongea na mtoto wako?	_____ _____
5. Je, mtoto wako amewahi kupokea elimu rasmi* nje ya Marekani? (Chekechea - daraja ya 12)  _____ Ndio _____ La  "Elimu rasmi" si mafundisho katika kambi za wakimbizi ama program zingine zozote za watoto zisizo rasmi.	Kama ndiyo, ni lugha gani ambazo maagizo yalitolewa? _____ Kwa miezi mingapi? _____
6. Mara ya kwanza kwa motto wako kuenda shule Marekani ilikuwa lini? (Chekechea - Kiwango cha 12)	_____ Mwezi                      Siku                      Mwaka

**\*WAC 392-160-005:** "Lugha msingi" humaanisha lugha ambayo inatumwa sana na mwanafunzi (haimaanishi na wazazi, walezi, au wengine) kwa mawasiliano katika eneo la makazi la wanafunzi.

Note to district: A response of a language other than English to question #2 OR question #3 triggers ELL placement testing.

## **Madhumuni ya Utafiti wa Lugha Msingi**

Utafiti wa Lugha ya Msingi hupewa wanafunzi wote wanaojisajili katika shule za Washington. Maelezo yafuatayo yatafaa katika kujibu baadhi ya maswali unayoweza kuwa nayo katika fomu hii.

### **Madhumuni ya Utafiti wa Lugha ya Msingi ni yapi?**

Sababu kuu ya Utafiti wa Lugha ya Msingi ni kusaidia kutambua wanafunzi ambao wanaweza kusaidiwa katika kukuza stadi muhimu za lugha ya Kiingereza zinazoweza kuwafaa darasani na pia wanaoweza kupewa huduma nyingine. Fomu hii sharti ijazwe kwa umakini na ukweli kwani inaweza kuathiri ufaafu wa mwanafunzi kwa huduma anazohitaji kuhitimu shuleni. Tathmini inaweza kuwa lazima ili kutambua ikiwa lugha ya ziada na usaidizi wa kiakademia unahitajika. Hakuna mwanafunzi atakayesajilishwa katika program yoyote ya kukuza lugha ya Kiingereza kutumia majibu yahii fomu tu.

### **Kwa nini mnauliza kuhusu lugha ya msingi ya mwanafunzi na lugha nyingine zinazotumiwa nyumbani?**

Maswali Hyo mawili kuhusu lugha za mwanafunzi yanatusaidia kutambua:

- Ikiwa mwanafunzi wako anahitaji usaidizi katika kujifunza Kiingereza, na
- Ikiwa wafanyakazi katika shule wanafaa kujua habari za lugha nyingine zinazotumiwa na wanafunzi nyumbani.

Lugha ya msingi ya mtoto wako inaweza kuwa tofauti na ile atumiayo katika mawasiliano nyumbani sasa. Majibu ya maswali haya mawili yatasaidia shule katika kutoa mafunzo yafaayo kwa mahitaji ya kibinafsi ya mtoto pamoja na kusaidia katika mahitaji ya mawasiliano yanayoweza kutokea. Wanafunzi waliojifunza lugha ya Msingi isiyo Kiingereza wanaweza kupewa huduma nyinginezo. Hata wanafunzi wanaozungumza Kiingereza vizuri pia huweza kuhitaji usaidizi katika kukuza stadi za lugha zinazohitajika katika kufaulu shuleni.

### **Kwa nini mnauliza mahala pa kuzaliwa kwa mtoto?**

Maelezo haya yanasaidia eneo la shule na serikali kubaini ikiwa mwanafunzi anatimiza hali ya uhamiaji ili kufadhiliwa na serikali. Hii inatumika hata ikiwa wazazi wote wa mwanafunzi ni raia wa Marekani, lakini mwanafunzi alizaliwa nje ya Marekani. Fomu hii haitumiki kubaini wanafunzi ambao hawako katika sajili.

### **Kwa nini mnauliza kuhusu elimu ya awali ya mwanafunzi wangu?**

Maelezo kuhusu elimu ya mwanafunzi yatasaidia kuhakikisha kwamba elimu ya mwanafunzi ndani nanje ya Marekani inatumika katika mapendekezo yoyote yanayofanywa katika kushiriki kwenye mipango ya huduma za eneo. Habari za elimu ya mwanafunzi pia husaidia kutathmini ikiwa mwanafunzi anapiga hatua kulingana na viwango vya serikali kwa kulingana na elimu yake ya awali.

Shukrani kwa kutoa taarifa inayohitajika katika utafiti wa Lugha ya Msingi. Wasiliana na eneo la shule yako ikiwa una maswali ya ziada kuhusu fomu hii au kuhusu huduma zinazopatikana katika shule ya mtoto wako.